

# 5 Miamba ya matumbawe

Ameinyanya mbingu juu na kuweka mizani ya vitu vyote, ili msivunje mizani hiyo. Toweni uzito na vipimo vya haki. (Qur'an 55:1-9)

## Matumbawe ni nini?

Miamba ya matumbawe ni mojawapo ya vitu vya kuvutia katika maumbile ya dunia! Zamani baadhi ya watu walifiki kuwa matumbawe yalikuwa aina ya mawe, lakini sasa wanaelewa kuwa matumbawe ni mkusanyiko wa wanyama wadogo sana wanoitwa 'polipu' (polyps) ambao wana kiunzi cha mfupa mgumu kwa nje mithili ya jiwe. Polipu wamehusiana na jejeta (mdudu wa bahari wa yavuyavu) na anemoni na kama wao wana vikia vyenye kuchoma ambayo wanaitumia kwa kulia 'planktoni' – mimea na wanyama wadogo sana wanaoeleya katika mikondo ya maji. Lakini matumbawe yanakula kwa namna nyingine ya pekee. Ndani ya seli za polipu kuna chembe za uhai (seli) za aina maalumu za mwani mdogo zinazoitwa. Kama ilivyo mimea yote mwani mdogo inatumia mwangaza wa jua, maji na hewa ya ukaa ili kutengeneza chakula (mchakato huu unaitwa usanisi mwanga au kwa kitaalamu (photosynthesis)). Sukari hii baadaye hugawanwa kati ya polipu ambaye ni mwenyeji wao. Faida yake ni kuwa polipu hulinda mwani mdogo dhidi ya wanyama wanaokula wengine na kutoa virutubisho pamoja na hewa ukaa. Rangi ya asili iliyomo ndani ya chembe za uhai za mwani ambazo zinayofanya mwangaza wa jua zina rangi inayong'aa sana.


Aina nyingi kabisa za matumbawe huota vyema mahali ambapo joto la bahari ni kuanzia nyuzi joto 23 - 29 sentigredi na hayawesi kuishi katika maji yaliyo na joto la chini ya nyuzi joto 18 sentigredi. Pia yanahitaji maji safi yasiyochafuka ambayo yanapata mwangaza wa jua mwangi na yenye mkusanyiko wa chumvi asilimia 3 - 4. Mahitaji haya maalum yanamaanisha kuwa aina nyingi sana za matumbawe na miamba hupatikana katika bahari za nchi za joto kwenye kina cha mita 2 - 30.

## Mwamba wa matumbawe ni nini?

Ni umbo la jiwe kama kiunzi cha mfupa wa polipu ambayo hufanyika kutokana na kalisiamu kaboneti chokaa inayowekwa na polipu wanapokua. Polipu wanapokufa, mifupa yao hubaki na polipu wengine huota juu ya mifupa mitupu, kwa hiyo tabaka jembamba la juu ya matumbawe linalongara ndilo lililohai. Baada ya muda mkusanyiko wa mifupa hii hukua na kufanya umbo kubwa la jiwe linaloitwa koloni la matumbawe. Makoloni ya matumbawe ya aina mbalimbali hukua katika sura tofauti, yaliyotoa matawi kama miti, kama rafu tambarare au kama maduara. Katika kipindi cha karne nyingi makoloni mbali mbali ya ukubwa tofauti, na maumbo na umri tofauti hukua pamoja, na hili hugeuka kuwa mwamba wa matumbawe. Zanzibar inazo kilomita 90 za mraba za mwamba wa matumbawe wa aina tatu. Miamba iliopinda (fringing reefs) inayopakana na ufukwe unaotenganishwa na mkondo mdogo baina yao. Miamba vizuizi (barrier reefs) imetenganishwa na ufukwe na wangwa, na miamba mabaka (patch reefs) ni miamba midogo, ya hapa na pale inayopatikana katika nyanga zenye mchanga.



Mwamba wa matumbawe ya Chumbe Island Coral Park © Oskar Hendrikson



Muundo polipu wa matumbawe  
imechorwa © Patterson Clark /  
Washington Post

## Kwa nini miamba ya matumbawe ni muhimu?

**Bioanuai** – miamba ya matumbawe ni mojawapo ya mifumo ekolojia tofauti iliyopo kwenye dunia yetu. Kuna spishi zipatazo 845 za mtumbawe yanayojenga miamba duniani kote, ambazo huwapatia makazi maelfu ya samaki wa miamba, chaza na kombe, kaa, kamba koche, spongi na mwani. Miamba ya Zanzibar ni makazi ya mamia ya spishi za samaki wa miamba ya mawe. Bustani ya matumbawe ya kisiwa cha Chumbe lina eneo lililohifadhiwa la Bahari lenye ukubwa wa 0.4 km<sup>2</sup>, lina zaidi ya matumbawe 200 na hawapungui spishi 432 za samaki.

**Chakula** – Samaki hutoa asilimia 60 ya protini ya wanyama inayoliwa Zanzibar, na kwa hiyo samaki ni chanzo muhimu cha chakula cha kisiwa hiki. Wengi wa

samaki hawa wanalazimika kuishi sehemu ya maisha yao katika **miamba ya matumbawe**.

**Kipato** – Uvubi ni shughuli kuu ya kiuchumi katika vijiji vya pwani, vikiwa kwa uchache na wavubi wapatao 34,000 katika Zanzibar. Wavubi wa Zanzibar huvua samaki wapatao tani 24,000 kila mwaka.

**Uzuri wa kimaumbile** – Sura na rangi tofauti zinazopendeza za **miamba ya matumbawe** na samaki wa matumbawe ni kivutio kizuri sana kwa watalii kuja Zanzibar kuzamia kwa kutumia gesi na kupiga mbizi. Utalii unatoa ajira si chini ya ya watu laki moja wa Zanzibar na asilimia 20 ya pato la taifa la Zanzibar.

**Hifadhi** – **Miamba ya matumbawe** hutoa kizuizi cha Kimaumbile baharini ambacho huwahifadhi watu wa eneo la pwani na **fukwe** za Zanzibar dhidi ya mmomonyoko na mafuriko kutokana na mawimbi ya dhoruba.

**Kupunguza kaboni** – **Polipu** wa matumbawe hufanya mifupa yao ya chokaa kutokana na kalisiamu (calcium) na kaboni (carbon) iliyoyeyuka katika maji chumvi. Mchakato huu, unaojulikana kama upunguzaji wa kaboni, husaidia kupunguza wingi wa hewa chafu katika hewa na kwa hiyo hupunguza kasi ya mabadiliko ya hewa.

### Tishio la miamba ya Zanzibar.

**Miamba ya matumbawe** imekabiliwa na matishio au hatari mbalimbali, hasa zinazotokana na shughuli za binaadamu.

**Uvubi wa kupindukia na uvubi mbaya** – Mahitaji ya samaki yanaongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu na idadi ya watalii. Uvubi wa kupindukia wa samaki, pweza, kaa na kamba ni jambo linalotia wasi wasi. Katika maeneo mengine ya Zanzibar, idadi ya samaki, kombe na chaza wa biashara wanapungua sana kiasi ambacho wavubi wanawapata wachache. Jambo hili linaleta matatizo zaidi. Kwa mfano samaki aina ya pono hula matumbawe, ambayo huyasaza menoni mwao na kutoa mchanga katika kinyesi chao ambaa huchangia katika kukusanya mchanga. Vile vile njia nyingine za uvubi zinaharibu matumbawe, kama vile **baruti** utumiaji wa sumu na uvubi aina ya ‘kigumi’ njia ambayo wavubi hutumia majiti kuvunja matumbawe na kuwatoa samaki. Njia hizi ni haramu; zinaharibu maeneo makubwa ya miamba na kuua samaki wote waliopo, na sio samaki waliokusudiwa tu. Nyavi zinazokokotwa juu ya miamba zinaleta uharibifu mkubwa, zinapokokotwa juu ya mwamba, na kuinasa na kuivunja vipande vipande. Nyavi nyingi kubwa zimenasa katika miamba na kuachwa hapo hapo katika Zanzibar.



Mpiga mbizi akiondoa nyavi iliyotelekezwa kutoka kwenye **mwamba wa matumbawe** katika Zanzibar © Anne Tarvainen



Kuenea kwa kiti cha pweza katika mwamba wa kisiwa cha Pemba mwamba © Chris Bartlett

**Matukambe** – Aina hii ya kitu cha pweza wenye mikia mingi wanakula **polipu** wa matumbawe. Kwa kawaida wanyama wanaokula wengine, kama vile aina ya kombe linaloitwa triton, huwala hawa matukambe, na kupunguza idadi yao, lakini makombe ya triton hupendwa sana na watalii na kwa hivyo hukusanya kwa wingi na watu wanokusanya makombe, kwa hivyo wameondolewa katika sehemu nyingi na watu wanaofanya biashara ya mapambo ya makombe. Bila ya kuwepo wanyama wanaokula wengine, husababisha mripuko wa maelfu ya matukambe haya ambayo, hufunika miamba na kusababisha uharibifu mkubwa.

**Kuogelea kwa kioo na kupiga mbizi** – **Polipu** wa matumbawe wanahisi upesi wanapoguswa na utapogusa koloni la matumbawe japo kidogo tu, **polipu** hizo hufa baada ya siku chache. Watu wanaogelea majini na wapiga mbizi ambaa hawana hadhari hurusha mchanga na kuharibu **polipu** na uharibifu mbaya zaidi hutokea wanapoyakanyaga matumbawe au kukaa juu yake. Inawezekana pia kukojoa majini na kuijipaka kwa waogoleaji aina ya mafuta ya kuzuia jua ‘sunscreen’ kuna athari mbaya kwa **miamba ya matumbawe** ambayo hutembelewa na watalii wengi.

**Mashua** – Mashua zinapokwama miambani, huvunjika na kuua matumbawe wakati mashua hizo zinapochukuliwa na mawimbi. **Kutia nanga** kwenye matumbawe pia kunaleta madhara makubwa kwa sababu sio tu kwamba nanga huvunja matumbawe, lakini pia mnyororo hufanya hivyo unapoyumba. Wenye mashua wanaua matumbawe vile vile wanapoyakanyaga.

### **Ulikua unajua...?**

- Matumbawe mengi yaliyopo yana umri wa katи ya miaka 6,000 na 9000!
- Matumbawe mengi yanakula planktoni (mimeti na wanyama wadogo sana wanaoishi majini) nyakati za usiku, hujificha vikia vyaonyakati za mchana ili wasiliwe na samaki au kuhifadhi mwani mdogo zisipate mwangaza wa jua amba wanauhitaji kwa ufanyakaji wa chakula!
- Ingawaje miamba ya matumbawe huchukua asilimia moja tu ya dunia inapatia makazi robo (asilimia 25) ya samaki wote duniani!
- Thamani ya miamba ya matumbawe duniani inafikia dola bilioni 30 za Marekani!
- Thuluthi moja ya spishi zote za matumbawe duniani zimeorodheshwa kama zipo hatarini kutoweke katika orodha ya IUCN ya orodha ya spishi zilizomo katika hatari yakutoweka.

### **Uchimbaji wa matumbawe na utengenezaji chokaa –**

Matumbawe yaliyo hai yanachimbwa na kutengenezwa chokaa kwa ajili ya ujenzi katika baadhi ya sehemu. Hiki ni kitendo cha uharibifu mkubwa, uharibifu wa makazi muhimu ya miamba ambayo huchukua miongo kadha kuyarudisha. Tatizo jengine ni kwamba tanuri / tanu zinazotumika kwa kutengeneza chokaa zinatumia mkaa wa mikoko, na kupelekea uharibifu zaidi wa rasilimali asili za pwani ya Zanzibar.

**Kukusanyika kwa mchanga** – Kila ardhi inapokatwa miti na mikoko inapokatwa kwa ajili ya kupata makazi (nyumba), na kilimo, ndiyo udongo zaidi unapoondoka kwenye ardhi na kwenda baharini hasa nyakati za mvua nyingi na kuyasonga matumbawe yaliyopo karibu. Kuvua kwa wauv pia kunapelekea kukusanyika kwa mchanga kwa sababu matope laini yanakorogeka wakati wa kuvua.

**Uchafuzi wa mazingira** – Kila idadi ya watu na watalii wanaotembelea Zanzibar inapoongezeka na ndivyo wingi wa maji machafu, mafuta, uchafu wa kemikali za takataka yatokayo majumbani zinavyoingia baharini. Haya yote yanaharibu matumbawe na viumbe wengine wa baharini.

**Kupauka kwa matumbawe na mabadiliko ya hali ya hewa** – Mabadiliko ya hali ya hewa yana athari nyngi kwa miamba ya matumbawe. Licha ya kuwa maji huwa ya moto zaidi, lakini hali ya hewa mbaya hutokeea mara kwa mara. Kwa mfano, hutokeea dhoruba kali zaidi – ambazo hukata vipande vya matumbawe, kuvuruga matope na mchanga na kupunguza viwango vya chumvi. Maji yanapokuwa ya moto kupita kiasi, tumbawe wa polipu hutoa mwani mdogo katika seli za uhai. Matumbawe hai upata rangi zao zinazoonekana kutokana na mwani huu kwa hiyo baada ya kutolewa matumbae huwa na rangi nyeupe inayong'ara. Tokeo hili linaitwa upaukaji. **Kupauka kwa matumbawe** ni jambo baya kwa sababu polipu hupata asilimia 90 ya chakula chao kutokana na mwani. Mara maji yanapokuwa baridi, yanaweza kula tena 'mwani', lakini maji yanapoendelea kuwa ya moto, polipu hufa haraka. Upaukaji wa matumbawe limekuwa jambo linalotokea mara kwa mara, na matokeo haya yanaathiri maeneo makubwa zaidi na miamba ya kina cha maji kikubwa kwa kila mara. Ugonjwa wa miamba pia unaongezeka katika baadhi ya matumbawe yenye hali ya joto zaidi.

**Kufanyika kwa tindikali katika bahari** – Ongezeko la hewa chafu ya kabondioidi katika anga inalopelekea mabadiliko ya hali ya hewa pia hufyonzwa na bahari ambako huchanganyika na chumvi iliyoyeyuka na kuifanya bahari kuwa na asidi / tindikali. Baadaye huiyeyusha chokaa ya mifupa ya matumbawe na kuifanya laini zaidi kwa matumbawe kujenga mifupa yao. Kuvunjika kwa miamba kutokana na tindikali ni jambo linalotia wasiwasi sana.

### **Tunawezaje kuhifadhi na kulinda miamba yetu ya matumbawe?**

Kama tulivyokwisha kuona, miamba ya matumbawe ni sehemu muhimu sana ya mazingira yetu. Tunayatengemea kwa mambo mengi. Matumbawe ni muhimu sana lakini pia ni rahisi kuvunjika na yanaweza kuharibika kwa urahisi kwa hiyo ni lazima tufanye kila tuwezalo na tushirikiane kuyalinda na kuyahifadhi.

Waogegeaji, wapiga mbizi na watumilaji gesi chini ya bahari wawe waangalifu wasiguse matumbawe na katu wasisimame juu ya miamba! Ni muhimu kukaa mbali na matumbawe, na kuwa na tahadhari usiyapige mateke matumbawe au kuvuruga mchanga.

Waendeshaji mashua na ngalawa wakae kwenye maji ya kina kirefu, na sio, kwenye miamba ya maji haba, na watie nanga kwenye mchanga au watumie boyo lililotulia kuweka alama ya wapi wafunge au kuweka nanga.

Wavuvi lazima waepuke au waache kutumia njia za uvuvi zinazoharibu miamba ya matumbawe: iwapo itaharibiwa samaki watatoweka. Wavuvi washirikiane na (watu) wengine katika jamii katika kusimamia rasilimali kwa kushirikiana, kwa mfano, kwa kuanzisha eneo linalohifadhiwa na jamii ili kuwalinda samaki.

### **Tembea ujione!**

- Tembelea maeneo ya hifadhi Zanzibar, mengi yana mipango ya elimu kwa ajili ya skuli, jamii, watalii na mengineyo.
- Tembea kwenye ufukwe wenyewe mawe wakati wa maji kupwa unaweza kuona vitumbawe vinaota katika vidimbwi vyenye mawe.
- Ongea na wavuvi wa eneo lako kuhusu mahali yalipo miamba ya matumbawe na jinsi uvuvi uliyobadiika katika miaka kadha.

**Kitunze kidumu** – Maeneo ya Bahari yanayohifadhiwa (MPAs) ambazo rasilimali asili za bahari ni zoni zinazohifadhiwa dhidi ya shughuli zenyeharibifu. Hatua za kuchukua ili kuhifadhi maeneo hayo zinaweza kujumuisha kupiga marufuku njia za uvuvi zinazoharibu au kupunguza idadi ya watalii wanaoruhusiwa kuzamia kwa kutumia gesi chini ya bahari au kupiga mbizi ili kulinda matumbawe ambayo ni rahisi kuvunjika pamoja na **makazi** mengine ya baharini. Faida yake ni kuwa samaki watapata mahali pa kukaa ambapo wanawenza kukua kwa haraka na kuzaa. Jambo hili kwa kweli linawanufaisha wavuvi kwa sababu huongeza idadi ya samaki katika sehemu za karibu kufikia mita 500 kutoka eneo la hifadhi zinazovuliwa kutokana na samaki kuhamia kwenye sehemu hizo! Matumbawe na idadi ya samaki inafuutiliwa na kuangaliwa, na matukambe wanaondolewa wakati wa kuzuka (wakiwa wengi). Kwa sasa kunasehemu sita za Hifadhi ya Bahari Katika Zanzibar: Kisiwa cha Chumbe (Kilichoanzia 1994, km<sup>2</sup> 0.4), Mnemba-Ghuba ya Chwaka (ikiwemo Hifadhi ya Kisiwa cha Mnemba (1997, km<sup>2</sup> 0.15), Hifadhi ya Ghuba ya Menai (1995, km<sup>2</sup> 467), Hifadhi ya Kisiwa cha Changuu-Bawe (2010), Hifadhi ya Kisiwa cha Tumbatu (2010) na hifadhi ya Mkondo wa Pemba (Ikiwemo Hifadhi ya Kisiwa cha Misali (1998, km<sup>2</sup> 23)). Maeneo mazuri ya Hifadhi ya Bahari zinaonesha muamko katika maeneo na jamii ziliomo ambazo zinategemea **miamba ya matumbawe**, kuhusu umuhimu na faida ya **miamba ya matumbawe** na jinsi gani tunaweza kuhifadhi vizuri.

Pia tunaweza kuyalinda matumbawe kwa kuitia shughuli za **ufukweni**. Usinunue au kuuza matumbawe au makombe makubwa kama ukumbusho **spishi** za makome mengi makubwa tayari ni wanyama walijomo hatarini ya kutoweka na kombe la aina ya baragumu lina jukumu / kazi muhimukatika kuhifadhi matumbawe dhidi ya matukambe!

Misitu, mikoko na nyasi bahari zote hufanya mchanga, matope na udongo utulie zaidi, kwa hiyo tunapaswa kuyahifadhi makazi haya ili kuzuia takataka zisiingie matumbawe na kuyasokota. Kwa mfano, tumia njia ya kupanda tena miti iliyokatwa kwa ajili ya kuni na sio kukata mikoko.



**Maeneo ya Hifadhi ya Bahari ya Zanzibar**  
© Nell Hamilton

### Kitunze kidumu!

- Kamwe usisimame juu ya miamba ya matumbawe!
- Usitupe taka baharini au ufukweni weka taka vizuri; zipunguze, zitumie tena, zirudishe kutengeneza vitu.
- Usitumie njia za uvuvi zenyeharibifu mazingira wala usinunue samaki waliokamatwa kwa mabomu/baruti au uvuvi wa sumu au njia nyengine za kuharibifu mazingira.
- Epuka kununua chokaa iliyotengenezwa kwa kuchoma matumbawe hai – tumia vitu vyengine bora kama vile matofali ya udongo, kuni zinaoweza kusarifika, au chokaa iliyotengenezwa kutoka maeneo ya mabaki ya miyamba ya matumbawe na wafahamishe wenzako jinsi wanavyoweza kuepuka shughuli zinazoharibu miamba ya matumbawe.
- Ripoti shughuli haramu za uvuvi kwa viongozi/vyombo vinavyohusika. Uharibifu wa matumbawe ni kuharibifu maisha ya watu wa Zanzibar, sasa na baadaye.
- Washawishi viongozi wa eneo kwa kuhifadhi na kulinda zaidi miamba ya eneo lako.
- Usiokote, kununua wala kuuza makombe hasa makombe aina ya baragumu.